UHURU UK 4

# Halmashauri nchini zaagizwa utoaji wa chanjo za mifugo

**Na MWANDISHI WETU**

HALMASHAURI za wilaya ambazo zimekuwa hazitoi chanjo za mifugo, zimeagizwa kuanza kufanya hivyo mara moja kuanzia Julai mwaka huu.

Pia, zimetakiwa kutumia chanjo zinazozalishwa nchini ili kudhibiti magonjwa ya mifugo.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alitoa agizo hilo juzi, wilayani Kongwa Mkoa wa Dodoma, wakati akizindua chanjo ya kudhibiti ugonjwa wa sotoka ya mbuzi na kondoo kitaifa inayozalishwa na kiwanda cha Hester Biosciences Africa Limited kilichopo Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani.

Alisema kuanzia Julai, mwaka huu atakuwa akipokea taarifa ya kila halmashauri namna inavyotekeleza utoaji chanjo za mifugo.

Waziri Ndaki aliwataka maafisa mifugo katika halmashauri hizo, kuhakikisha wanatumia chanjo zinazozalishwa ndani ya nchi zikiwemo za Taasisi ya Chanjo Tanzania (TVI), inayomilikiwa na serikali pamoja na chanjo zinazozalishwa na viwanda vinavyomilikiwa na sekta binafsi.

"Halmashauri ambazo hazitoi chanjo kwenye mifugo yao, kuanzia Julai mwaka huu, mifugo yote ianze kuchanjwa na mimi nitaanza kupokea taarifa ya kila mwezi ya uchanjaji wa mifugo yetu, ili tujue baada ya mwaka mmoja, mifugo yetu yote itakuwa imechanjwa?

"Pia, chanjo zitakazotumika ziwe zinazozalishwa hapa nchini, hatuna sababu ya kuagiza chanjo kutoka nje ya nchi," alisema.

Katika uzinduzi huo wa chanjo kitaifa dhidi ya ugonjwa wa sotoka ya mbuzi na kondoo, Waziri Ndaki alisema ni muhimu kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini kwani husaidia kuwa na soko la uhakika, hivyo kukuza pia ajira na kwamba chanjo za mifugo zinazozalishwa nchini zinatengenezwa katika mazingira rafiki.

Aidha, alishukuru kiwanda cha 'Hester Biosciences Africa Limited' kwa msaada wa chanjo 700,000 zenye thamani ya sh. milioni 245 walioipatia wizara kama mchango wao kwa jamii na kutoa wito kwa wadau wengine katika sekta ya mifugo kushirikiana na serikali kutatua changamoto zilizopo katika sekta hiyo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Hester Biosciences Africa Limited, Dk. Furaha Mramba, alisema kiwanda hicho kitazalisha aina 37 za chanjo za mifugo ili kuhakikisha magonjwa yote ya mifugo yanakuwa na chanjo za kuyadhibiti ukiwemo ugonjwa wa homa ya nguruwe ambao wataanza kuufanyia utafiti wa kisayansi.

Dk. Mramba alisema kiwanda kinatarajia kuzalisha dozi zisizopungua bilioni 1.5 kwa mwaka pale kitakapokuwa kinazalisha chanjo zote zilizokusudiwa na matarajio ni kuuza asilimia 20 ya chanjo hizo ndani ya nchi na asilimia 80 zinategemewa kuuzwa katika nchi jirani za Afrika Mashariki na nyingine katika nchi za Afrika.

Aliongeza kuwa, chanjo hiyo itapatikana nchini kote ambapo katika uzinduzi huo, Wilaya ya Kongwa imepatiwa bure dozi za chanjo hiyo, wafugaji hawatagharamia kiasi chochote cha fedha huku kwa wilaya zingine bei elekezi ya chanjo hiyo ni sh. 350 hadi 400 kwa mbuzi na kondoo.

Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Hezron Nonga, alisema kumekuwa na changamoto za uwepo wa magonjwa mbalimbali ya mifugo, mengi yanadhibitiwa kwa njia ya chanjo ukiwemo ugonjwa wa sotoka ya mbuzi na kondoo na lengo ni kuutokomeza.

Profesa Nonga alisema chanjo ni njia nafuu katika kudhibiti magonjwa ya wanyama na kwamba, tiba ni bei ghali endapo mnyama akiugua kwa sababu wafugaji wamekuwa wakiingia gharama kubwa kuwatibu wanyama.

**CHANJO**

**MIFUGO**

Aliwataka maafisa mifugo katika halmashauri hizo kuhakikisha wanatumia chanjo zinazozalishwa ndani ya nchi

Rais Samia Mei 22, mwaka jana na ubunifu, fanyeni hivyo, leteni mawazo Balozi Noel Kaganda.

UHURU UK 15.

# UZINDUZI



**WAZIRI** wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (wa pili kulia), akizindua chanjo ya kitaifa dhidi ya ugonjwa wa sotoka ya mbuzi na kondoo, mjini Kongwa mkoani Dodoma, juzi. Kulia ni Mbunge wa Kongwa, Job Ndugai. (Picha na Wizara ya Mifugo).

UHURU

Serikali yae

UHURU Uk 15

# Serikali yaelekeza halmashauri kudhibiti magonjwa ya mifugo

**Na MWANDISHI WETU**

HALMASHAURI za wilaya ambazo hazitoi chanjo za mifugo, zimeagizwa kuanza kutoa huduma hiyo mara moja kuanzia Julai, mwaka huu.

Pia, zimetakiwa kutumia chanjo za mifugo zinazozalishwa nchini, ili kudhibiti magonjwa ya mifugo na kukuza soko la chanjo hizo.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, katika Wilaya ya Kongwa, mkoani Dodoma.

Aliyasema hayo alipokuwa akizindua chanjo ya kudhibiti ugonjwa wa sotoka ya mbuzi na kondoo kitaifa inayozalishwa na kiwanda cha Hester Biosciences Africa Limited kilichopo Wilaya ya Kibaha, mkoani Pwani.

Alisema kuanzia Julai, mwaka huu, atakuwa akipokea taarifa ya kila halmashauri namna inavyotekeleza utoaji wa chanjo za mifugo.

Ndaki aliwataka maofisa mifugo katika halmashauri hizo kuhakikisha wanatumia chanjo zinazozalishwa ndani ya nchi zikiwemo za Taasisi ya Chanjo Tanzania (TVI), inayomilikiwa na serikali na zile zinazozalishwa na viwanda vinavyomilikiwa na sekta binafsi.

"Halmashauri ambazo hazitoi chanjo katika mifugo yao, kuanzia Julai, mwaka huu, mifugo yote ianze kuchanjwa na nitaanza kupokea taarifa ya kila mwezi ya uchanjaji wa mifugo yetu, ili tujue baada ya mwaka mmoja mifugo yetu yote itakuwa imechanjwa?,"

"Na pia, chanjo zitakazotumika ziwe zinazozalishwa hapa nchini na hatuna sababu ya kuagiza chanjo kutoka nje ya nchi," alisema.

Scanned with CamScanner

Shumba Mjini, Wilaya ya Micheweni Pemba, jana. (Picha na Ikulu).

UHURU UK 18.



NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (katikati) akipata maelezo kutoka kwa Meneja Msaidizi wa Mradi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Abdallah Fedes (kulia) kuhusu ramani ya eneo la Kijiji cha Msomera lililotengwa kwa ajili ya wafugaji kutoka katika hifadhi hiyo, kijijini hapo, Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga, juzi. (Picha na Wizara ya Mifugo).

Scanned with CamScanner



Mwema).

HABARI LEO UK 8.

# Halmashauri zisizotoa chanjo ya mifugo zaonywa

Na Anastazia Anyimike

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki ameziagiza halmashauri ambazo hazitoi huduma ya chanjo kwa mifugo kufanya hivyo kuanzia Julai mwaka huu.

Waziri pia amesisitiza chanjo zitakazotumika ziwe ni zile zinazozalishwa hapa nchini.

Ndaki aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa chanjo ya ugonjwa wa sotoka kwa mbuzi na kondoo iliyotengenezwa kwa mara ya kwanza hapa nchini na kiwanda cha Hester Bioscience Afrika Ltd uliofanyika wilayani Kongwa.

Alisema magonjwa ya mifugo yamekuwa kikwazo katika uzalishaji na biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya Tanzania, hivyo amezitaka halmashauri zote kutoa chanjo kamilifu.

Pia aliagiza ripoti ya idadi ya mifugo na aina ya chanjo iliyotolewa kupelekwa kwa Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo kila mwezi.

"Serikali imekusudia kutokomeza magonjwa ya mifugo na kuifanya Tanzania kuwa huru kwa magonjwa ambayo yamedumu kwa muda mrefu. Hivyo wataalamu, wafugaji na viongozi mna wajibu wa kusimamia sheria, kanuni na taratibu za udhibiti wa magonjwa kama ilivyoelekezwa na wataalamu."

Ndaki pia aliwaelekeza wataalamu wote wa mifugo ngazi ya wizara, mikoa, wilaya na kata kuhakikisha uchanjaji wa mifugo unatekelezwa kikamilifu kulingana na kalenda ambalo ni takwa la kisheria.

"Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo hakikisha unasimamia jukumu hili na niwe napata ripoti ya chanjo kila mwezi. Wakurugenzi wa halmashauri na kampuni za kutoa chanjo nunueni na mchanje mifugo kwa kutumia chanjo zilizozalishwa hapa nchini kwa kuwa zimetengenezwa na vimelea vilivyopo nchini," alisisitiza.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo, Profesa Hezron Nonga alisema serikali imeweka mikakati ya kutokomeza ugonjwa wa sotoka kwa mbuzi na kondoo kama ilivyokuwa kwa ng'ombe ifikapo mwaka 2025 ikiwa ni kabla ya mwaka 2030 uliowekwa na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE).

Alisema bei elekezi ya chanjo hiyo ni Sh 350 kwa mifugo na kuwataka wataalamu kutotoza zaidi ya bei elekezi.

Mkurugenzi Mkuu wa Kiwanda hicho, Tina Sokoine alisema kiwanda hicho ni kikubwa kwa ukanda wa Kusini mwa Afrika kinachotumia teknolojia ya kisasa.

Alisema kina uwezo wa kuzalisha aina 37 za chanjo kwa ajili ya kukinga ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku, punda, farasi na baadaye chanjo ya nguruwe.

Alisema kiwanda kinatarajia kuzalisha dozi zaidi ya bilioni 1.5 kwa mwaka kitakapokuwa kinazalisha chanjo zote zilizokusudiwa na asilimia 20 inatarajia kutumika ndani ya nchi na asilimia 80 kuuzwa nje.

Awali, Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Dk Furaha Mramba alisema chanjo ya magonjwa ya sotoka ya mbuzi na kondoo tayari imeshapata ithibati ya kimataifa na uzalishaji wa awali ni dozi milioni 35.

Alisema baada ya chanjo hiyo, kiwanda kitaanza uzalishaji wa chanjo za kuzuia mapele ya ngozi, ndui ya mbuzi na kondoo, homa ya mapafu ya ng'ombe, homa ya mapafu ya mbuzi na kondoo kabla ya Julai 2022 baada ya kupata ithibati.

Naye Mbunge wa Kongwa, Job Ndugai alishukuru Serikali kwa juhudi ya kuwafanya wafugaji wawe ni wenye tija na kwamba ugonjwa wa mifugo umekuwa ukiwakatisha tamaa wafugaji.

Scanned with CamScanner